

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 026 2322761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili umepangwa kuanza tarehe 2 Februari hadi tarehe 12 Februari, 2021. Shughuli zitakazofanyika katika Mkutano huu ni kama ifuatavyo:-

1. Maswali

Katika Mkutano huu wastani wa maswali 125 ya kawaida na Maswali 16 ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yanatarajiwa kuulizwa na Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 45 (1) na 44 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

2. Hotuba ya Rais

Kwa mujibu wa Kanuni ya 36 (3) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kujadili Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Mbili.

3. Kamati ya Mipango

Aidha, Katika Mkutano huu, Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango ili kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Bunge hukaa kama Kamati ya Mipango katika katika Mkutano wa Mwezi Oktoba – Novemba kila mwaka isipokuwa kwa Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya. Kwa kuwa Mkutano wa Novemba, 2020 ulikuwa wa Kwanza wa Bunge hili, hivyo Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango katika Mkutano huu wa Pili.

Ratiba yote ya Mkutano wa Bunge inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.bunge.go.tz

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,

Ofisi ya Bunge,

DODOMA.

1 Februari, 2021